

Haki ya Msingi ya Usawa mbele ya Sheria.


TAWLA ipo kwa kukusaidia wewe kuelewa nini hasa maana ya Haki hii.

Endapo una swali lolote, au unahitaji msaada, tafadhali tuandikie "TAWLA", S.L.P. 9460, Dar es Salaam Tanzania.



DESIGN NA MICHORO WALTER LEMA
(DESIGN AND DRAWING)
REDISIGN HELMUT PFINDEL

IMEFADHILIWA KWA PAMOJA
NA ROYAL DANISH EMBASSY
IMEFADHILIWA NA MEDICAL MISSION SUPPORT
UNITED STATES INFORMATION SERVICES (USIS)



IMETOLEWA NA KUTAYARISHWA NA CHAMA CHA
WANAWA KE WANASHERIA TANZANIA (TAWLA)

WOSIA

ANDIKA WOSIA KUEPUSHA USUMBUFU NA MATATIZO KWA WALE WANAObAKIA - HASA FAMILIA YAKO

1. WOSIA Ni NINI?

Neno WOSIA lina maana zifuatazo

- (i) Ni maandishi au maneno yanayotamka mtu akielezea jinsi mazishi yake yatakavyokuwa, anaweza kuelezea mahali atakapozikwa n.k.
- (ii) Agizo atoalo mtu wakati wa maisha yake lihusulo namna mali yake itakavyofanywa wakati akifariki
- (iii) Andiko lenye wosia alioutoa Mwosia.

MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA KUANDIKA WOSIA

- (i) Mwosia awe na uwezo wa kuandika wosia. Yaani asiwe chini ya miaka 18 ya kuzaliwa. Pia awe na akili timamu.
- (ii) Iwapo Mwosia anajua kusoma na kuandika ni lazima kuandika wosia wake. Wosia huo ushuhudiwe na masha hidi wawili. Inapobidi mmojawapo awe mtu wa ukoo wa mwosia. Iwapo mwosia hajui kusoma na kuandika ni lazima wosia huo ushuhudiwe na watu wanne - wawili kati yao wakiwa ni watu wa ukoo wa mwosia.

Wosia uandikwe kwa kalamu ya wino au isiyofutika au upigwe chapa.

Tarehe ya kuandikwa wosia ni ya muhimu hiyo iandikwe.

Wosia utaje kuwa mwosia ametia sahihi yake mbele ya mashahidi wake, wakati mmoja kwa hiari yake mwenyewe na kwamba andiko hilo linashuhudiwa kuwa ni wosia wake ambao utatumika baada ya kifo chake Mwosia asiyejua kusoma au kuandika aelezwe kuhusu wosia wake.

Mwosia ataje msimamizi wa mali yake katika wosia. Iwapo mwosia ni mgonjwa wakati wa kuandika wosia, Daktari ahusishwe ili kuthibitisha kuwa mwosia alikuwa katika hali ya kuweza kuandika au kutoa wosia ijapo alikuwa mgonjwa.

Warithi hawapashwi kujua mwosia amewausia nini Wosia unaweza kuhifadhiwa sehemu yoyote yenye usalama kuepusha uwezo wa kufanyiwa mabadiliko na mtu asiye mwosia. Hivyo sehemu kama vile Benki, makanisa Mahakamani n.k. zinafaa kutunzia.

ZINGATIA: WOSIA KATIKA SHERIA ZA KIISLAMU

Mwosia hawezi kuusia mali yake yote. Kisheria anaruhusiwa kuusia 1/3 ya mali yake 2/3 ya mali iliyo-baki inagawanywa kwa taratibu za dini hii.

HATI YA WOSIA INAWEZA KUANDIKWA HIVI

WOSIA

Mimi

Ninayeishi

Nikiwa na akili timamu NAFUTILIA MBALI WOSIA zangu ambazo niliwahi kutengeneza au kuandika kabla ya tarehe ya leo na kutangaza kuwa huu ndio Wosia wangu wa mwisho

Tarehe

Na kwa wosia huu ninamrithisha:

(1)mke wangu nyumba iliyopo

(2)mtoto wetu wa kwanza wa Kike gari TZB No

(3)mtoto wangu wa kiume nyumba na sha mba lililoko

(4)mtoto wangu wa kike n.k.

Kwa wosia huu ninamteuakuwa msimamizi na muamana wa Wosia huu.

Kwa kushuhudia hayo yalioelezwa ninaweka saini yangu katika siku na mwaka ulioelezwa hapo juu.

Imewekwa sahihi na.....)

Mwosia mbele yetu katika muda huu)

kutokana na matakwa yake mwenyewe nasi)

tunaweka majina yetu hapa chini kama mashahidi

1. Jina la Shahidi

Sahihi

Kazi

Tarehe

2. Jina la Shahidi

Sahihi

Kazi

Tarehe